**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**
**BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA MITIHANI YA 33 YA PSPTB

**Dodoma 25 Februari, 2026**

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi **(**PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, mitihani ya kitaaluma ya 33 ya PSPTB inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe **11/05/2026** mpaka tarehe **15/05/2026**. Waombaji wenye sifa na nia ya kuomba kufanya mitihani hii wanaelekezwa kufanya usajili wa mitihani hii kupitia **https://registration.psptb.go.tz** na pia kuhudhuria madarasa ya mafunzo kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **19/04/2026**. Mitihani hii itafanyikia katika vituo vilivyoko **Dar es Salaam, Moshi, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Arusha** na **Zanzibar** kama inavyooneshwa katika dirisha la usajili.

**WAOMBAJI WAFUATAO WANA SIFA YA KUFANYA MITIHANI YA KITAALUMA YA MEI, 2026**

(1) Wahitimu wote waliomaliza Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2025 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

(2) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya ununuzi na ugavi kwa ngazi za stashahada shahada na Astashahada au wenye sifa za kitaaluma kutoka Bodi / Mabaraza ya taaluma husika na yanayotambulika na PSPTB.

(3) Watahiniwa wa PSPTB waliomaliza mitihani ya kitaaluma ya Awali ngazi ya pili *(Basic Stage II)*, mitihani ya kitaaluma ngazi ya Msingi *(Foundation Stage I and II)*, Mitihani ya Kitaaluma ngazi ya kwanza, pili, tatu na nne *(Professional Stages I, II, III and PIV)* ndani ya miaka mitano kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala wa Kitaaluma.

(4) Watahiniwa wote wanaorudia baadhi ya masomo katika ngazi mbali mbali ndani ya miaka mitatu kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala mpya.

(5) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi katika sekta binafsi na umma pasipokuwa na cheti cha CPSP.

**NB.** Watahiniwa wanaorudia mitihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana *(Two Consecutive Blocs)* kwa masomo kuanzia mawili hadi sita tu, na kwa kuzingatia ratiba ya mitihani ya 33 ya PSPTB. Hivyo, wanaombaji wote wanaotarajia kufanya mitihani yao **wanashauriwa** kuangalia ratiba ya mitihani tajwa kabla ya kuomba kufanya mitihani hiyo.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia ***examinations@psptb.go.tz***

Digitally Signed By GODFRED MBANY
Wed Feb 25 22:30:54 EAT 2026

GODFRED MBANYI
**MKURUGENZI MTENDAJI**